# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 035 NOVEMBA 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



1. TMA NA SHIRIKA LA MSALABA MWEKUNDU TANZANIA WASAINI MAKUBALIANO YA MASHIRIKIANO YA UTOAJI ELIMU NA USAMBAZAJI WA TAARIFA ZA HALI YA HEWA

2. DKT. CHANG'A APEWA JUKUMU LA KUSIMAMIA BODI YA SAYANSI KATIKA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC)




3. FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2023



## KITAIFA

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA NA SHIRIKA LA MSALABA MWEKUNDU TANZANIA WASAINI MAKUBALIANO YA MASHIRIKIANO YA UTOAJI ELIMU NA USAMBAZAJI WA TAARIFA ZA HALI YA HEWA

**Dar es Salaam**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS) wamesaini rasmi makubaliano ya mashirikiano ya utoaji wa elimu na usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kwa jamii ili kuweza kuwafikia kwa usahihi na wakati. Mkataba huo wa mashirikiano ulisainiwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu TMA na Makamu Mwenyekiti Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabia Nchi (IPCC) Dkt. Ladislaus Chang'a, na Katibu Mkuu wa TRCS Bi. Lucia Pande, Dar es Salaam,Tarehe 13 Novemba, 2023.

"TMA na TRCS zimeendelea kuimarisha zaidi mashirikiano ya kiutendaji ili kuweka nguvu za pamoja katika kuokoa maisha ya watu na mali zao kutokana na majanga

yanayotokana na hali mbaya ya hewa, ambayo yanaendelea kuongezeka kwa idadi na ukubwa wa matukio. Makubaliano haya ni moja ya utekelezaji wa mkakakati



wa Taifa wa kukabiliana na madhara yatokanayo na athari za El Nino". Alisema Dkt. Chang'a.

Katika hatua nyingine, Bi. Lucia Pande alifafanua kuwa TMA na TRCS wamekuwa wakifanya kazi kwa pamoja kwa kipindi kirefu, hivyo katika hatua za kongeza ufanisi wa utendaji kazi wa pande zote mbili, tumefikia makubaliano ya pamoja ya kuweka ushirikiano kimaandishi. Hatua hii ni uhimu sana kwa TRCS katika kuimarisha matumizi sahihi ya taarifa za kisayansi za hali ya hewa zinazotolewa na TMA katika kujiandaa na kuchukua hatua stahiki wakati wa majanga.



## KIMATAIFA

# DKT. CHANG'A APEWA JUKUMU LA KUSIMAMIA BODI YA SAYANSI KATIKA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC)

**Geneva, Uswisi**




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)", Dkt. Ladislaus Chang'a, amepewa jukumu la kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Sayansi katika Jopo la IPCC.

Dkt. Chang'a alipewa jukumu hilo katika mkutano wa 66 wa viongozi wa Jopo la IPCC (Sixty-sixth IPCC Bureau) uliofanyika Geneva, Uswiss tarehe 15 na 16 Novemba, 2023. Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa ni kujadili maandalizi ya utekelezaji wa shughuli za IPCC katika Tathmini ya Saba ya IPCC ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC Seventh Assessment Cycle - AR7). Mkutano huo ni wa kwanza tangu uongozi mpya wa IPCC uchaguliwe katika uchaguzi

uliofanyika mwezi Julai 2023. Uongozi wa IPCC una jumla ya viongozi thelathini na nne (34), Dkt. Chang'a ni miongoni mwa viongozi hao ambapo alichaguliwa katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti akiwa miongoni mwa Makamu Wenyeviti watatu wa IPCC.

Bodi ya Sayansi ya IPCC atakayoisimamia Dkt. Chang'a inaundwa na Makamu Wenyeviti wote watatu wa IPCC ambao ni Dkt. Ladislaus Chang'a (Tanzania), Prof. Ramón Pichs-Madruga (Cuba), na Prof. Diana Ürge-Vorsatz (Hungary). Miongoni mwa shughuli zitakazoambatana na jukumu hilo jipya alilopewa Dkt. Chang'a ni: kusimamia programu ya IPCC ya ufadhili wa mafunzo (IPCC Scholarship Programme); kuratibu ushiriki wa wanasayansi chipukizi (Young Scientists) katika masuala ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi; na kuwakilisha jopo la IPCC katika programu ya WMO ya utafiti "(World Weather Research Programme (WWRP) ".

Jukumu jipya alilopewa Dkt. Chang'a la kusimamia Bodi ya Sayansi ya Jopo la IPCC pamoja na fursa za mpya za mashirikiano na WMO ni mwendelezo wa kuaminika kwa TMA na Tanzania kimataifa. Hii inatokana na mchango mzuri unaotolewa na wataalamu wa TMA katika nafasi mbalimbali wanazohudumu, ikiwa ni pamoja na vikosikazi vya WMO. Mafanikio haya yanaendelea kuitangaza Tanzania kimataifa na kuimarisha zaidi mahusiano mazuri ya kidiplomasia kati ya Tanzania na nyingine katika utoaji wa huduma za hali ya hewa.

Katika hatua nyingine, Dkt. Chang'a alishiriki katika mkutano wa kuwajengea uwezo Wawakilishi wapya wa Kudumu wa Nchi katika WMO (Permanent Representatives of Members with WMO) uliofanyika Geneva, Uswis kuanzia tarehe 20 hadi 22 Novemba, 2023. Kupitia mkutano huo, alipata pia fursa ya kukutana na baadhi ya viongozi katika vitengo vya WMO ambapo walijadili maeneo mapya ya ushirikiano na TMA kupitia programu za WMO, ikiwa ni pamoja na WMO kutambua mifumo iliyobuniwa na wataalamu wa TMA ili itumike katika huduma za hali ya hewa.

IPCC ni Chombo cha Umoja wa Mataifa kinachosimamiwa na WMO na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (United Nations Environmental Programme- UNEP). Chombo hicho kilianzishwa mwaka 1988 kwa jikumu la kusimamia sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi ambapo Jopo hilo hufanya tathmini za mwenendo wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi na kuandaa taarifa za tathmini (Climate Change Assessment Reports) ambazo zina mchango muhimu katika kufanya maamuzi ya kukabiliana na madhara yanayosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi. Tangu kuanzishwa kwake, IPCC imeandaa taarifa sita za tathmini, ambapo tathmini ya sita (IPCC Sixth Assessment cycle) ilianza mwaka 2015 na kukamilika mwaka 2022. Uongozi mpya wa IPCC utasimamia Tathmini ya Saba ya IPCC ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi inayotarajiwa kuanza mapema mwaka 2024 na kukamilika mwaka 2030.

# JARIDA LA MWEZI

06 TOLEO NA. 035 NOVEMBA 2023

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

## FAHAMU ZAIDI

### HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI DISEMBA, 2023

Katika kipindi cha mwezi Novemba 2023, mvua za Msimu, 2023/2024 zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka mvua zinatarajiwa kuendelea. Hata hivyo, ongezeko la mvua linatarajiwa nchini. Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi inatarajiwa kuendelea husuan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Katika kipindi hiki, vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa kati wiki ya kwanza na ya pili.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Vipindi vya mvua vinavyoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Novemba,2023. **Aidha ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Vipindi vya mvua vinavyoambatana na ngurumo kwa baadhi ya nyakati vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya tatu ya mwezi.** |

JARIDA LA MWEZI

07 TOLEO NA. 035 NOVEMBA 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# BIDHAA NA HUDUMA ZA TMA

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA KWA SEKTA YA MAZINGIRA

Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania (TMA) inatoa huduma za hali ya hewa zinazosaidia sekta ya Mazingira kudhibiti athari zinazohusiana na hali mbaya ya hewa. Huduma hizi zinatolewa kwa kufuata na kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Mamlaka hutoa huduma zifuatazo za hali ya hewa kwa shughuli za mazingira; -**

(a) Taarifa za jumla za hali ya hewa.
(b) Takwimu na taarifa za ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi. Takwimu za uchafuzi wa angahewa.
(c) Takwimu za klimatolojia kama ilivyoanishwa kwa eneo maalum ikiwemo matukio ya hali ya hewa yaliyokithiri.
(d) Utabiri wa hali ya hewa mahsusi (maalum) na tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa.
(e) Kasi na mwelekeo wa upepo
(f) Ripoti za Sunami
(g) Huduma nyingine zozote inayohusiana.

**Wateja wa sekta ya mazingira hutumia huduma za hali ya hewa kwa shughuli zifuatazo za mazingira-**

(a) Kuweka msingi katika kupanga kwa ajili ya kupunguza upotevu wa mali na mali asilia na za kimazingira pamoja na mambo mengine ikiwemo kujua maeneo ya bahari ambayo umwagikaji wa mafuta unaweza kujitokeza na kufika katika mwambao.
(b) Uhifadhi wa mabaki yanayotokana na bidhaa zinazozalishwa au zinazotengenezwa kutoka viwandani kama vile mbolea na saruji pamoja na vitu vingine.
(c) Kupunguza uchafuzi wa mazingira.
(d) Tathmini ya athari na mkakati/mpango/sera katika kufanya tathmini kwa Mazingira.
(e) Udhibiti wa taka.
(f) Shughuli nyingine yoyote inayohusiana.






JARIDA LA MWEZI
TOLEO NA. 029
MEI 2023
TMA
1 ELIMU YA HALI YA HEWA YATOLEWA KWA WATU WENYE UHITAJI MAALUM
2 TANZANIA YAPEWA KIPAUMBELE UBORESHAJI WA MIUNDO MBINU YA HALI YA HEWA
3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2023


**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa



www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.